# MBIU - SHAWISHI
## Kwa Viongozi




## TANZANIA

UNAIDS

unicef
United Nations Children's Fund



# Mbiu ya mgambo ikilia ina jambo!

"Vita dhidi ya UKIMWI lazima vianze kwa kutooneana haya na kuwa wazi na wakweli. Kila mmoja ashiriki katika kubomoa ukuta na ukimya unaozunguka maradhi haya. Tunayoyasema kwa kunong'ona sasa tuyaseme kwa uwazi. Aidha tutambue na kukubali kwamba UKIMWI ni ugonjwa kama ugonjwa mwingine, hivyo tusiwabague hata kidogo, wala kuwanyooshea kidole wala kuwacheka walio nao" - *Rais Benjamin Mkapa akitoa salamu. za Mwaka Mpya na Milenia Mpya, Desemba 31, 1999.*

# Dibaji

UKIMWI ni tatizo kubwa hivi sasa kuliko hata vita vinavyoendelea sehemu mbalimbali dunian. Kasi ya kuenea kwake inatisha!

Hapa Tanzania, inakadiriwa kuwa watu milioni moja tayari wana UKIMWI na wengine milioni tatu wameambukizwa virusi vya ugonjwa huo. Idadi ya watoto yatima kutokana na mzazi mmoja au wazazi wote kufariki dunia kutokana na ugonjwa huu inakadiriwa kuwa zaidi ya milioni moja. Ni nadra kumkuta Mtanzania ambaye hajapoteza ndugu yake wa karibu, jamaa au rafiki kutokana na UKIMWI.

Kwa mantiki hiyo basi, vita dhidi ya UKIMWI ni yetu sote, na viongozi wetu hawana budi kushika hatamu za uongozi katika mapambano. Wewe kiongozi silaha yako katika vita hii dhidi ya UKIMWI ni Mbiu-shawishi.

Mbiu-shawishi [kwa kiingereza *advocacy*] dhidi ya UKIMWI inalenga kukupa mwongozo na nyenzo zitakazokuwezesha kufahamu na kuchagua mbinu sabihi za kupigania mambo muhimu ill kupunguza kasi ya kuenea kwa ugonjwa huu, na matunzo bora ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Matokeo ya Mbiu-shawishi itakayofanywa kwa ufasaha na viongozi yawe ni kuleta mshikamano ndani yajamii ili kuchukua hatua madhubuti dhidi ya ugonjwa huu.

Katika mwongozo huu, zipo taarifa muhimu kuhusu UKIMWI ambazo kiongozi unapaswa kuzifahamu kabla ya kuingia katika uwanja wa mapambano. Wewe kiongozi, tumia mwongozo huu ili kutoa Mbiu-shawishi itakayopunguza kasi ya kuenea kwa UKIMWI. Mbiu ya kiongozi hufika mbali kwa sababu hata wahenga walisema, *Mbiu ya mgambo ikilia...*

## I.0 VIONGOZI KATIKA MBIU-SHAWISHI DHIDI YA UKIMWI

Rais Benjamin Mkapa, Waziri Mkuu Mheshimiwa Frederic Sumaye na Mwenyekiti wa Bodi Kuhusu UKIMWI, Alhaji Ali Hassan Mwinyi wameanza kuwa wazi kuhusu tatizo hili kubwa la kijamii. Hizi ni ishara nzuri za kuimarisha mkakati wa Mbiu-shawishi katika ngazi nyingine.

Kwa kutumia Mbiu-shawishi, viongozi hao wametoa changamoto kubwa kwa viongozi wengine ngazi zote katika kuzungumza bayana kuhusu UKIMWI kwa sababu wanasiasa wengi wa ngazi mbalimbali za uongozi huuonea aibu sana

ugonjwa huu kwa hofu ya kubezwa na wananchi wanapowaasa kubadili mienendo na tabia kuhusu ngono za uzembe. Hatua hii italeta mabadiliko makubwa katika sera, mipango, sheria na msukumo dhidi ya UKIMWI.

## 2.0 HATUA ZA MBIUMSHAWISHI

**Kwanza:** Lijue tatizo au suala Iinalotakiwa kufanyiwa Mbiu-shawishi. Kwa mfano: Desturi ya kurithi wajane au ngono baina ya jinsia moja inaongeza kasi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Kutokana na desturi hizo idadi kubwa ya watu sasa wana virusi vya UKIMWI na wengine wamekwisha fariki dunia.

**Pili:** Baada ya kulijua tatizo, watambue washiriki wenza ili kwa pamoja mtatue tatizo.Ukiwa kiongozi, hauna budi kufahamu nani anapaswa kutoa efimu hiyo au kaondoa mila na desturi potofu. Washiriki wenza wanaweza kukupa nyenzo za kufanyia Mbiu-shawishi kama vile takwimu sahihi kuhusu tatizo lililopo na athari zake kiafya na katika maendeleo.

**Tatu:** Anza kutoa Mbiu-shawishi kwa washiriki wenza ili waweze kuwashawishi na kuwahamasisha wananchi au walengwa wabadilike. Kama serikali imeshaweka sera ya kupiga vita mila ya kurithi wajane, ni wajibu wa kiongozi kupigia debe utekelezaji wa sera ili kuwepo na mabadiliko ya dhati.

**Nne:** Jenga ushirikiano na wananchi kupitia vyombo vya habari vya kisasa na vya asilI. Vyombo hivyo vitaweka bayana nani anayeendeleza mila na desturi hizo licha ya kuwepo kwa sera au sheria ndogondogo zinazozuia vitendo hivyo. Vilevile vitatangaza taarifa kuhusiana na athari mbaya za vitendo hivyo kwa afya za wananchi na kwa maendeleo yajamii kwa ujumla.

**Tano:** Shirikisha watu maarufu kwenye ngazi zote katika Mbiu-shawishi yako kwani wanaweza kukusaidia kwa sababu wana nafasi zao katika jamii.

**Sita:** Fuatilia (follow-up and monitor) na pima matokeo (evaluate) ya Mbiu-shawishi ili kuweza kurekebisha makosa na kuongeza ufanisi katika hatua nyingine ya utekelezaji. Ni muhimu **Utathmini**, **Uchambue** kabla ya kuanza **Utekelezaji** wa mkakati na mipango mingine.

## Kisanduku Namba I:

### MFANO WA MBIU-SHAWISHI
### HOJA: KUVUNJA UKIMYA KUHUSU UKIMWI

**Kujenga hoja:**
Utafiti umeonyesha kwamba vijana wengi hujihusisha na ngono isiyo salama wakiwa na umri mdogo (hata miaka tisa) kutokana na jamii (wazazi na jirani) kushindwa kuzungumza na vijana kwa uwazi na kwa ufasaha kuhusu suala zima la ngono na mabadiliko ya miili ya vijana.

**Lengo Kuu**
Kuvunja ukimya juu ya masuala yahusuyo ngono na uhusiano wake na UKIMWI

**Lengo mahsusi**
Kuwaongezea maarifa viongozi wa ngazi mbalimbali wa kiserikali, kisiasa, kidini na kijamii juu ya njia ya kuvunja ukimya uliopo kuhusu suala la ngono hasa kwa vijana.

**Walengwa**
Viongozi wa ngazi mbalimbali kutegemeana na anayeongoza Mbiu-shawishi.

**Washiriki- wenzi**
Wazazi, vijana na jamii kwa ujumla, vyombo vya habari hasa redio, mashirika yasiyo ya serikali, viongozi wa dini, wawezeshaji rika, wasanii.

**Wanufaika**
i)Vijana (ii) Watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI

**Ujumbe maalum**
Wakati umefika wa kuwa wazi na kuongea na watoto na vijana wetu kuhusu masuala ya ngono kama njia ya kubadilika tabia na kupiga vita

**Mbinu za Utekelezaji**
- Kuitisha mkutano na viongozi wa makundi ya vijana katika eneo husika na kutoa ujumbe ili wasaidie kuusambaza kwa mbiu-shawishi
- Kutafuta upendeleo na kuzengea vyombo vya habari ili viweze kufanya mahojiano na vijana kujua mawazo yao ya kuudhibiti ugonjwa wa UKIMWI
- Mikutano ya uhamasishaji
- Vipeperushi
- Kutumia vikundi vya sanaa kwenye mikutano ya viongozi

**Upimaji wa Utekelezaji**

- Mara ngapi kwa mwezi au mwaka viongozi wa juu wa serikali au dini wanazungumza kwa wazi masuala haya?
- Je, redio imeandaa na kurusha hewani vipindi vingapi, kama ni magazeti, makala ngapi kwa kipindi fulani; karna ni televisheni, vivyo hivyo.
- Idadi ya wanaoishi na virusi waliojitokeza tangu kuanza kwa mkakati huu.
- Idadi ya watu wanaokwenda kupata ushauri nasaha kwenye vituo vya afya na hata upimaji kujua hali kama kuna virusi vya UKIMWI au la.
- Idadi ya wawezeshaji rika waliopata mafunzo na kuwasaidia vijana wenzao.
- Idadi ya vituo vya vijana na matumizi yake

## 2.1 Mambo yanayokusaidia kuamua ufanye Mbiu-shawishi au la

I. Jambo unalotaka kupigia debe lina mguso kwa watu wengi?
2. Jambo hilo liwe linaungwa mkono na wengi
3 . Je, Mbiu-shawishi uliyoichagua itakusaidia kudhibiti kuenea kwa virusi vya UKIMWI?
4. Je, una takwimu za kukaziajambo lako? (wataalam wakusaidie)
5. Je, hoja anayoijenga itaeleweka kwa urasi?
6. Je, ni rahisi kawasilisha hoja na kuwasiliana na walengwa kulingana na mila na desturi?
7. Je. kuna vikundi vingine vinavyotetea hoja kama yako?
8. Iwezeshe jamii husika kuelewa masuala mengine ya kitaifa yenye mwelekeo huo huo.
9. Kuimarisha mahusiano na vikundi visivyo vya serikali na kawajibika kwa vyombo vya ngazi ya chini
10. Itoe nafasi ya kuendeleza mipango

N.B.:Iwapo hoja yako itajibu maswali zaidi ya matano, unaweza kufanya mbiu-shawishi.

## 3.0 KUTUMIA MBIU-SHAWISHI KUWABADILI WANAOFICHA NA KUKATAA KUWEPO TATIZO LA UKIMWI

Mbiu-shawishi ya viongozi katika mapambano dhidi ya UKIMWI inalenga kutokomeza tabia mbaya kwa baadhi ya viongozi ya kukanusha kuwepo kwa

ugonjwa huu katika maeneo yao au kuonyesha kuwa tatizo "siyo kubwe" kama inavyofikiriwa.

Tabia hii ya kuficha tatizo pia imewakumba wananchi wa kawaida. Baadhi hawawezi kueleza kuwa miongoni mwa familia zao wamo ambao wamekufa kwa UKIMWI. Mbiu-shawishi itakayofanywa na viongozi inaweza kusaidia kufutilia mbali tabia hiyo. Mbiu-shawishi itasaidia pia kuzifanya programu zote za kupambana na UKIMWI ziungwe mkono na wote wenye majukumu na wajibu wa kutoa maamuzi.

## 3.1 Mbiu-shawishi ilenge kutokomeza ubaguzi na kejeli

Baadhi ya jamii hapa nchini zinaamim kwamba kuwatenga na kuwakejeli watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI kunasaidia kupunguza kasi ya kuenea kwa ugonjwa wa UKIMWI katika maeneo yao wanamoishi. Imani hii ni potofu na haina msingi wowote na inasababishwa na ukosefu wa elimu

jinsi virusi vya UKIMWI vinavyoambukiza. Ni vyema basi, Mbiu-shawishi ya viongozi ikalenga katika kutokomeza tatizo hili.

## 3.2 Mbiu-shawishi kwa kutumia watu waishio na virusi

Njia mojawapo ya kupambana na tabia hii ya kuukataa ukweli ni kuwawezesha watu wenye virusi vya UKIMWI kujitangaza hadharani. Wakifanya hivyo, watu wanaokataa kuwepo kwa UKIMWI, wataamini kuna UKIMWI.

Viongozi wa vikundi au mashirika yasiyo ya kiserikali na watu waishio na virusi vya UKIMWI wanaweza kufanya Mbiu-shawishi inayoweza kuleta mafanikdo makubwa.

- Wanaweza kupigia debe uundwaji wa vikundi vingi vya aina hiyo nchi nzima na kutaka viungwe mkono kisheria. Vikundi hivi vitakuwa na mtandao hadi Viiijini.
- Watahamasisha wenzao kutoa ushauri nasaha kwa wasiopimwa. Uzoefu wao wa kuishi kwa muda mrefu kwa kufuata masharti na miiko ya wataalam itawapa nguvu na kuwafanya watu wengine wawe na ari ya kujitokeza kupimwa wakijua kuna faraja na matumaini ya kuishi muda mrefu.

## 3.3 Walengwa katika mbiu shawishi

A. *Watoto na Vijana:*

[Kwa sababu wengi wao wameathirika]

- Idadi kubwa ya watoto na vijana hawana taarifa sahihi kuhusu UKIMWI, masuala ya ngono na mabadiliko ya miili yao.
- Wengi wao hawana stadi zinazowawezesha kufanya maamuzi ya busara na kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

B. *Sekta ya afya:*

Sekta hii ina majukumu ya kulinda na kuboresha huduma za afya.

- Upatikanaji na utoaji wa dawa za magonjwa ya ngono kama kaswende ni muhimu.
- Idadi kubwa ya hospitali hapa nchini hazina watoa ushauri nasaha na huduma maalum kwa watu wenye virusi vya UKIMWI kama wanawake wajawazito wenye virusi vya UKIMWI, na hata kama washauri hao wapo, idadi kubwa hawana elimu ya kutosha juu ya utoaji ushauri nasaha kwa watu waishio na virusi vya

C. *Viongozi wa DinilMadhehebu:*

Kundi hili linaongoza waumini wengi wenye rika, elimu na jinsi tofauti. Mahubiri dhidi ya UKIMWI yana nafasi kubwa katika kuwashawishi waumini wao kuacha vitendo vinavyoweza kupelekea kupata virusi vya UKIMWI.

D. *Taasisi binafsi na mashirika yasiyo ya kiseilkaii:*

Viongozi wa taasisi hizi, pamoja na mambo mengine, wanaweza kufanya yafuatayo:-

- Kuendelea kutoa elimu dhidi ya UKIMWI kwa makundi mbalimbali katika jamii;
- Kutoa takwimu za maambukzo ya virusi vya UKIMWI na athari zake katika maendeleo;
- Kuhamasisha jamii kutowatenga na kuwahudumia waathirika wa zUKIMWI.

E. *Sekta ya elimu:*

Walimu wengi wanafariki dunia kutokana na ugonjwa wa UKIMWI na bado wale waliobakia hawana stadi za kutosha za kuuelewa ugonjwa wa UKIMWI na hatimaye kuwaelimisha Wanafunzi wao. Wanafunzi wengi wanakosa haki ya kufahamu kuhusu UKIMWI kutokana na uzito uliopo katika kuzungumzia UKIMWI kwa uwazi kuanzia ngazi ya familia hadi shuleni.

# 4.0 MAMBO MUHIMU KUHUSU UKIMWI

## 4.1 Maana

UKIMWI ni kifupi cha maneno: Upungufu wa Kinga Mwilini unaosababishwa na virusi vijulikanavyo kwa Kiingereza kama Human Immunodeficiency Virus (HIV)

Virusi vya UKIMWI vinaishi katika majimaji yote ya mwili kama shahawa majimaji ya ukeni na katika damu. Kwa sababu hiyo, vinaweza kuhamia katika mwill wa mtu mwingine kwa njia ya tendo la ndoa (ngono) au kuchanganyikana kwa damu.

## 4.2 Hali ya Ugonjwa

Tangu kuzuka kwa UKIMWI mwaka 1981 duniani, inakadiriwa na Mpango wa Umoja wa Mataifa wa UKIMWI (UNAIDS) kuwa hadi Desemba mwaka 1999, jumla ya watu milioni 47 walikuwa wameambukizwa virusi duniani kote. Asilimia 70 ya watu hao wenye virusi wamo barani Afiika.

Kulingana na taarifa za Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP) za mwaka 1998, Tanzania ilikuwa na wagonjwa wa UKIMWI wapatao milioni moja na Watanzania wengine milioni tatu wanaishi na virusi vya UKIMWI.

## 4.3 Virusi vya UKIMWI huambukizwaje?

- Kujamiana kwa kutumia njia ya kawaida (vaginal) au njia ya haja kubwa (anal).
- Kuwekewa damu kutoka kwa mtu mwenye virusi
- Kuchangia vifaa vyenye damu yenye virusi kama sindano, wembe, vifaa vyenye ncha kali au miswaki.
- Mama mjamzito humwambulaza mtoto wake ama wakati akiwa tumboni au wakati wa kujifungua na wakati wa kumnyonyesha.

## 4.4 Huwezi kuambukizwa virusi...

- Kwa kumgusa mtu mwenye virusi, kumkumbatia, kumbusu.
- Kuchangia vyombo kama sahani na vikombe vyakunywea maji na mtu mwenye virusi vya UKIMWI.
- Kwa kuumwa na mbu
- Kutumia choo au jiko la kupikia pamoja na mtu mwenye virusi.

## 4.5 Dalili za Uambukizo

Idadi kubwa ya watu wanaoambukizwa virusi vya UKIMWI hawaonyeshi dalili mara moja baada ya kuambukizwa. Inaweza kuchukua muda mfupi au mrefu hata miaka kumi kwa dalili za kwanza za maambukizo kujitokeza kulingana na uwezo wa mwili kujikinga na maradhi.

**Dalili Kuu**

- Kupunguauzitowamwiliasilimia 10 kwa mwezi mmoja
- Homa za mara kwa mara kwa kipindi cha mwezi mmoja
- Kuhara kwa zaidi ya mwezi mmoja

**DatiUnyingine**

- Kukohoa kusikoisha kwa zaidi ya mwezi mmoja
- Mwasho wa ngozi
- Kuugua mkanda wa jeshi (Shingles)
- Kuvimba kwa tezi kusikopona
- Kupoteza kumbukumbu na kupagawa

## 4.6 Magonjwa Makuu yanayoambatana na UKIMWI

i. Kifua kikuu (TB)
ii. Magonjwa ya zinaa (STD)
iii. Vidonda sehemu za siri
iv. Kutoa usaha ukeni au uumeni

## 4.7 Jinsi ya kuzuia maambukizo ya virusi vya UKIMWI

Virusi vya UKIMWI havienei wala kuambukizwa kwa njia ya hewa, maji a chakula kama ilivyo kwa magonjwa mengi ya kuambukiza. Yafuatayo in mamb muhimu ya kuzingatia:-

**i. Epuka kufanya mapenzi yasiyo salama**

Zaidi ya asilimia 80 ya watu wenye virusi vya UKIMWI wameambukizwa kw kufanya mapenzi yasiyo salama kwa njia ya kawaida ya ukeni au ya haja kubw Kuacha kabisa kujamiiana kunapunguza kwa kiasi kikubwa uwezekano w kuambukizwa virusi vya UKIMWI.

**ii. Pima kwanza kabla ya kufunga ndoa na kuwa mwaminifu katika nd yako**

**iii. Ikishindikana kabisa, tumia mpira wa kiume au wa kike (kondom kufanya mapenzi**

**iv. Epuka tendo la kulawiti**

**v. Tumia sindano mpya au iliyochemshwa kila unapochomwa**
**vi. Tumia wembe mpya wakati wa kunyoa**
**vii. Kuwa mwangafifu na vifaa vya kung'olea meno**
**viii. Sisitiza mgonjwa wako aongezewe damu salama (isiyo na virusi vya UKIMWI)**
**ix. Kama ni mwanamke kabla ya kubeba ujauzito pima kwanza na ikiwezekana mshauri na mwenzio mkapime virusi vya UKIMWI, ili kuhakikisha mtoto anayezaliwa ni salamal**

## 4.8 Je kuna tiba dhidi ya UKIMWI

Mpaka sasa hakuna tiba wala chanjo dhidi ya UKIMWI. Wanasayansi duniani wanaendelea kutafata tiba. Dawa zilizopo ni za kupunguza makali ya ugonjwa huu. Dawa hizi, kwa kitaalam, (Anti Retrovirals) ni kama vile AZT, na kazi yake kubwa ni kupunguza kasi ya ugonjwa wa UKIMWI na kamwe hazitibu ugonjwa huu. Dawa hizi ni za gharama kubwa na hazipatikani kwa urahisi. Zipo pia dawa zinazopunguza uwezekano wa mama mjamzito kumwambukiza mtoto wake aliye tumboni, hata hivyo hizi nazo ni aghali.

### 4.9 Dawa za jadi

Matumizi ya mitishamba au dawa za asili yameonyesha kuondoa baadhi ya dalili za ugonjwa kwa watu wenye virusi. Hali hii imewafanya watu wengi na hasa waganga wenyewe wa jadi kaamini na kudai kuwa wanazo dawa za UKIMWI na kuwa unatibika. Waganga hawa hawana uwezo wa kisayansi kuchunguza kama mgonjwa hana virusi baada ya kutumia dawa. Kuna umuhimu wa ushirikiano baina ya waganga wa jadi na wataalam wa afya kutafiti dawa za jadi kwa kutumia vifaa vya kisasa.

### 4.10 Huduma kwa Wenye Virusi vya UKIMWI

Ukiwa kiongozi, una nafasi na uwezo mkubwa wa kuwashawishi wananchi unaowaongoza kuelewa na kukubali kuwa mtu anayeishi na virusi vya UKIMWI; au mgonjwa wa UKIMWI ni sawa na mgonjwa yeyote yule. Watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI wasitengwe, wahudumiwe na waheshimiwe. Hatua hii inasaidia watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI:

- Wasaidiwe kisaikolojia kwa kupewa ushauri nasaha.
- Watibiwe magonjwa "swahiba" yanayowashambulia kama vile kifua kikuu. Mengi ya magonjwa hayo yanatibika.
- Wapewe lishe bora na matunzo mazuri.
- Haki zao za kisheria kama urithi na haki ya kuamua vile wapendavyo kwa

kuzingatia sheria zilindwe.

## 4.11 Watoto na UKIMWI

**Mtoto ni nani?**

Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa, mtoto ni binadamu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18. Katika zama hizi za ugonjwa wa UKIMWI, takwimu zinaonyesha kwamba hapa Tanzania zaidi ya asilimia 60 ya waathirika wote wa UKIMWI ni watu wenye umri chini ya miaka 18 (watoto). Hali hii inalazimisha kila jamii kuandaa mkakati maalum wa kukabiliana na ugonjwa huu miongoni mwa watoto. Mkakati huu uzingatie zaidi haki kuu nne za msingi za Mtoto ambazo ni Kuishi, Kuendelezwa, Kulindwa na Kushirikishwa.

Ni vyema kuelewa kuwa ukosefu wa haki za msingi kama vile kulindwa hupelekea watoto kuambukizwa virusi vya UKIMWI. Na vile vile ugonjwa wa UKIMWI unaweza kusababisha mtoto kukosa haki zake za msingi. Mathalani kutokana na kuambukizwa virusi vya UKIMWI, mtoto ananyimwa haki ya kuendelezwa kwa kupatiwa elimu. Kutokana na mazingira hayo mawili, mikakati yoyote inayolenga watoto ni lazima kabla ya kuanza kutekelezwa ibainishe inalenga kutatua tatizo lipi. Kuwapa watoto haki zao ili kuwaepusha na UKIMWI au kuwaepusha na UKIMWI kwa kuwapatia haki zao za msingi.

Pamoja na kwamba watoto wote wana haki sawa, wapo watoto wanaohitaji mkakati wa pekee katika kuwaepusha na

◆ **Watoto walio katika mazingira magumu**

Kundi hili linajumuisha watoto waishio mitaani, walioko katika ajira (shambani, migodini, biashara na majumbani), ukahaba na masikini. Kundi hili lipo katika hatari ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI kapitia ngono isiyo salama ili kukidhi mahitaji yao kutokana na hali ngumu ya maisha inayowakabili.

◆ **Watoto wenye ulemavu**

Kundi hili lipo kwenye hatafi kubwa ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI kulingana na maumbile yao, ukosefu wa taarifa sahihi kuhusiana na UKIMWI au kwa kuonewa.

◆ **Elimu ya UKIMWI kwa watoto**

Ili watoto waweze kujiepusha na maambukizo ya virusi vya UKIMWI, elimu inaweza kutolewa kwa njia mbalimbali kuanzia ngazi ya familia (wazazi na

walezi), vyombo vya habari, waelimishaji rika, vikundi vya sanaa na maigizo. Vile vile waelimishaji kutoka mashirika yasiyo ya Kiserikali wanaweza kuwatembelea watoto katika maeneo waliyopo na kuwapa elimu na stadi za maisha.

## 5.0ATHARI ZA UKIMWI

### i. Sehemu za kazi

Ugonjwa huu unaathiri shughuti za kazi kwa njia nyingi zikiwemo:-

- Kupoteza watu wenye elimu na uzoefu mkubwa
- Kuondoka kazini ili kuwahudumia ndugu na jamaa na kuhudhuria mazishi ya watu waliokufa kutokana na UKIMWI
- Kuongezeka kwa gharama za kuajiri na mafunzo kwa wafanyakazi wapya
- Uzalishaji mdogo wa waajiriwa wapya. Inachukua muda mrefu hadi waajiriwa wapya kuwa wazalishaji wazuri kama wale waliokufa kwa ugonjwa huu.
- Kupanda kwa gharama za matibabu ya wafanyakazi pamoja na kuhudumia mazishi.

### ii. Huduma za Afya

- Nchi nyingi zimekumbwa na ongezeko la mahitaji ya huduma za afya wakati wakati ambapo pato la taifa linashuka kutokana na kupotea kwa nguvu kazi. Inakadiriwa kuwa hapa Tanzania, ifikapo mwaka 2005 mahitaji ya Vitanda hospitalini kwajili ya wagonjwa wa UKIMWI yataongezeka kwa kiasi kikubwa.

### iii Familia na UKIMWI

- Asilimia kati ya 30 na 50 ya pato (na rasilimali) la familia hutumika kumhudumia mgonjwa wa UKIMWI.
- Wanandugu katika familia hulazimika kuacha kazi zao ili kupata muda wa kutosha kumhudumia mgonjwa na hivyo familia nzima huathirika hasa kama chanzo kikuu cha mapato ndani ya familia ndiye anayeugua.
- Watoto yatima wanaathirika zaidi kwa kupoteza mzazi mmoja au wazazi wote wawili na wanandugu na wakati mwingine, watoto wenyewe kulazimika kuchukua nafasi ya kuwalea wadogo zao. Watoto hawa hupoteza mwelekeo na wakati mwingine huacha kuendelea na masomo.

### iii. Elimu

Elimu ni sekta nyingine iliyoathirika sana na ugonjwa huu. Uchunguzi wa Benki ya Dunia hapa nchini umeonyesha kuwa UKIMWI utasababisha vifo vya walimu 15,000 ifikapo mwaka 2010 na idadi hiyo itaongezeka kufikia

walipu 27,000 ifikapo mwaka 2020. Watoto, hasa wakike hulazimika kuacha shule kwa kukosekana fedha za kulipia ada na michango au sare au kulazimika kuchangia huduma za kifamilia majumbani.

**iv. Michezo**

Ugonjwa huu pia umetoa changamoto kubwa kwa viongozi wa michezo kurekebisha baadhi ya sheria za michezo ili kupunga kasi ya maambukizi wakati wa michezo. Kwa mfano, kwenye mchezo wa ngumi, sasa ni lazima kisheria kwa kila bondia kupimwa kwanza iwapo ana virusi vya UKIMWI au la kabla ya kumhusiwa kupigana.

## KIAMBATANISHO 1

## BAADHI YA MAMBO AMBAYO VIONGOZI WANAWEZA KUFANYIA MBIU-SHAWISHI

1. Kuhamasisha watu hasa vijana na wanaume kukubali na kujitokeza kupata ushauri nasaha na baadaye kupimwa kwa hiari kujua kama wana virusi au la.
2. Jamii ikubali kuwatunza, kuwalinda, kawahudumia wagonjwa wa UKIMWI.
3. Jamii ishirikiane na waliojitangaza kuwa na virusi vya UKIMWI katika kampeni ya kupambana na UKIMWI.
4. Kuhakikisha haki za msingi za mtoto zinalindwa ili aweze kuishi na kusbiriki katika mambo yanayomhusu.
5. Kupinga upimaji bila ridhaa kujua hali ya kuwepo au kutokuwepo virusi kwa watu mbalimbali hasa wasioweza kujitetea wenyewe.
6. Kuhakikisha Bunge linaweka sheria zitakazowabana watu wanaowabagua wenye virusi vya UKIMWI sehemu za ajira.
7. Kukemea tabia na mienendo inayopelekea maambukizi ya virusi vya UKIMWI hasa miongoni mwa vijana na makundi maalum yanayoathirika upesi.
8. Kuhimiza kuwepo ushirikiano wa watu, taasisi na vikundi mbalimbali na jumuia ya kimataifa katika mipango dhidi ya UKIMWI.
9. Kupigania kuendelea kuwepo bajeti inayolenga mahsusi mipango ya UKIMWI kama dawazinazo zuia kuambukizwa virusi kutoka kwa mama mjamzito mwenye virusi vya UKIMWI; kwenda kwa mtoto na kila hospitali ya wilaya na kituo cha afya iwe na vifaa vya kupimia hali ya virusi na wataalam wa ushauri nasaha.
10. Kuanzisha mfuko wa taifa wenye lengo la kuwawezesha vijana kujiajiri kama njia ya kupunguza matamanio na kuepuka mazingira yaletayo maambukizi ya

virusi vya UKIMWI.

11. Kuhimiza wizara hasa ya afya na sheria kuangalia mara kwa mara mabadiliko ya sheria na kanuni ili kuzuia maambukizi ya UKIMWI.
12. Kusimamia utekelezaji wa sheria ndogondogo za serikali za mitaa na vijiji ili kuzuia maambukizo
13. Kupigania uundwaji wa Kamati Maalum ya Bunge kuhusu UKIMWI ili kuratibu shughuli za mbiu-shawishi zinazofanywa na wabunge majimboni mwao.
14. Kutekeleza agizo la serikali la kuhakikisha suala la UKIMWI linakuwa ajenda ya kudumu katika vikao vya ngazi zote.
15. Kufanya UKIMWI kama Ajenda ya Uchaguzi Mkuu wa Rais na wabunge na kushawishi kila chama kiweke katika ilani yake mikakati dhidi ya ugonjwa huu.
16. Kuendeleza kampeni ya kitaifa ya stadi za maisha kwa wanafunzi wa shule zote za msingi na sekondari nchini.
17. Kuifanya Siku ya UKIMWI Duniani iwe siku ya kutathmini utekelezaji wa mipango ya kudhibiti UKIMWI katika jamii husika.
18. Yatima ana haki ya kurithi, kusaidiwa na kutotengwa kielimu

## KIAMBATANISHO NA. 2

## MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA KUHUSU UKIMWI

*SWALI:* *Je nawezaje kujiepusha na UKIMWI?*

**Kwa kuwa na mpenzi mmoja mwaminifu ambaye hajaambukizwa virusi vya UKIMWI.*

**kwa kutumia kondom wakati wote kama una mpenzi zaidi ya mmoja*

**Kwa kutibu haraka magonjwa ya zinaa mara unapoumwa.*

**Kwa kuepuka sindano za uchochoroni. Hakikisha unachomwa sindano mpya kila unapolazimika kuchomwa.*

**Kwa kuhakikisha kuwa damu utakayoongezewa imepimwa kama haina virusi vya UKIMWI.*

**Kwa kuepuka kuchangia vifaa vya kunyolea, kutogea, kuchanjia na kung'olea meno.*

*SWALI:* *Je waweza kuzuia kuambukizwa UKIMWI kwa kuoga na kujisafisha mara baada ya kujamiiana?*

**JIBU:** Hapana, UKIMWI unaambukizwa wakati uleule wa kujamiiana,

kuosha au kusugua Uume au kutawaza uke haitasaidia kuzuia maarnbukizo.

*SWALI:* *Je mtu mwadilifu anaweza kupata UKIMWI?*

**JIBU:** Ndiyo, kwasababu watu waadilifu pia hujamiana, hudungwa sindano na wanaongezwa damu na kung'olewa meno.

*SWALI:* *Je waajiri wana haki ya kuwapima wafanyakazi wao UKIMWI?*

**JIBU:** Hapana. Hakuna sheria inayolazimisha upimaji wa virusi vya UKIMWI kabla ya kuajiriwa.

*SWALI:* *Je nifanyeje kama namfahamu mtu mwenye virusi vya UKIMWI?*

**JIBU:** Wachukulie kawaida kama mtu mwingine yeyote na kumbuka kwamba Hakuna hatari ya kuambukizwa UKIMWI kwa njia kama kusalimiana.

*SWALI:* *Watu wanaoishi na virusi vya UKIMWIwana haki na wajibu gani?*

**JIBU:** Watu wanaoishi na virusi vya ugonjwa wa UKIMWI wana haki sawa kama wengine ila wana wajibu wa kuhakikisha hawafanyi maambukizi ya ugonjwa huo makusudi au kwa uzembe.

*SWALI:* *Je wanawake ndio chanzo cha usambazaji wa virusi vya UKIMWI ?*

**JIBU:** Hapana. Virusi vya UKIMWI vinaweza kuambukizwa kutoka kwa mwanaume kwenda kwa mwaname au kutoka kwa mwanamke kwenda kwa mwanaume.

*SWALI:* *Kwanini tuendelee kuhimiza unyonyeshaji, wakati tunaambiwa kuwa unyonyeshaji unaweza kueneza virusi kwa mtoto.*

**JIBU:** Utaalam umeonyesha kwamba kutokunyonyesha mtoto maziwa ya mama aliyeambukizwa UKIMWI kuna athari zaidi kwa mtoto kuliko kumnyonyesha, hii ni kwa sababu maziwa ya mama yana virutubisho muhimu ambavyo itasaidia kuzuia maambukizo na kumuwezesha mtoto kukua vizuri.